*Makala hii ichapishwe*
*na isambazwe*

# Maelezo ya njia mpya za kupinga tohara kwa wanawake

***- IP -***

## 1. Utangulizi

Jawabu la mkutano wa 17 wa Kamati maalum ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia maswala ya watu wa Makabila ya Kiasili uliofanyika Geneva, Julai 26 hadi 30 1999, ni kuweka mikakati thabiti dhidi ya kutahiri wanawake. Lengo la ripoti hii ni kuunga mkono jitihada za kukabiliana na matatizo haya kwa njia mpya kabisa. Imeonekana kuwa vita dhidi ya kile kiitwacho "tohara ya wanawake" – tendo la ukatili la kuondoa kinembe na mara nyingi pia midomo ya uke *(labiae)* haikufikia lengo lake.

Imekadiriwa kuwa tohara ya aina hiyo inafanyika kwa wasichana zaidi ya millioni mbili kwa mwaka. Umri wao wakati wa kutahiriwa hutofautiana kufuatana na mila au mazoea kuanzia utotoni hadi utu uzima. Tunakabiliwa na mashaka ya kuchagua ama mila za utamaduni kwa upande mmoja au misingi ya haki za binadamu kwa upande mwingine. Inaonekana kuwa kuheshimu upande mmoja ni kutojali upande mwingine.

Hata hivyo uamuzi unaweza kuhalalishwa
kufuatana na sababu za tiba na za fikira.

## 2. Mfano

Mara nyingi katika nchi zinazoendelea ni tabaka la juu linalofuata mambo ya kisasa. Kwa mwenendo huu, watu wengine hudhani ni kupotea kwa utamaduni wenye thamani na mila. Lakini mara nyingine sababu zinaweza kuwa njema. Ni kweli kwamba jitihada zimefanywa kuondoa kabisa tohara kwa wanawake, ingawa mafanikio yamekuwa madogo, na imekuwa dhahiri hata kupiga marufuku sheria za nchi – kama Guinea, Niger na Sudan – ni vigumu kabisa.

Nchini Misri kwa mfano, asilimia 97 ya wanawake wote wanatahiriwa. Hii inaonyesha wazi ugumu wa swala hili katika mfumo wa maisha ya sasa. Hapo awali ilikubaliwa kuondolewa kwa kinembe ifanyike hospitalini. Lakini kutokana na kampeni ya kupiga vita tohara kwa wanawake, mpango huu ulikatazwa rasmi mwaka 1996.

Lakini nini ilitokea baadaye? Je, ulikuwa mwisho wa ukeketaji huko Misri?

Kwa bahati mbaya haikuwa hivyo. Matokeo ya kupiga marufuku mila hizi, ni kwamba tohara iliendelea kwa siri hata katika maeneo yasiyotambulika rasmi. Hivyo, nyembe zenye kutu zilitumika na matatizo yaliongezeka. Pia kutokana na ukosefu wa dawa, wasichana waliteseka vibaya. Mwaka 1997, serikali iliamua kurudisha huduma za kutahiri wasichana hospitalini.

## 3. Maswala ya kitamaduni

Tunajifunza nini kutokana na hayo? – Bila shaka kuna mambo ya kitamaduni ambayo hayakuangaliwa:

- Mila si rahisi kuondoa.
- Iko haja ya mambo ya utamaduni.
- Maswala hayo yasipozingatiwa hapatakuwepo na ufumbuzi wa tatizo hili.

Katika macho za kizungu, inaonekana – kama vile imekwisha fanyika kitambo – “Hatukubali utamaduni zenu. Mziondoe na muwe kama sisi“. Lakimi tunaona mahali fikira za aina hizi zimetufikisha – tatizo lilizidishwa badala ya kurekebisha.

Hoja za kitamaduni ni kizuizi kikuu katika mapambano dhidi ya ukeketaji. Mara nyingi, inaonekana dhahiri kuwa, hata wale wahusika ndiyo wanaoutaka utaratibu *wenyewe*. Na wakina mama wasipopenda kuendeleza zoezi hili kwa binti zao, wakina bibi hutumia njia nyingine za ujanja ama nguvu.

Kampeni dhidi ya kutahiri wanawake inaweza kufanikiwa tu ikiwa mambo yanayostawisha na kujenga utamaduni huu yanaeleweka. Jitihada zu kuondoa ukeketaji kisheria hazikufanikiwa, badala yake ubaya wake umezidishwa. Ni muhimu zibuniwe njia nyingine, mbali na sheria pekee yake ambazo zitazingatia umuhimu wa utamaduni. Hata hivyo, sababu za kuendeleza tohara kwa wanawake ni imani imara kwamba kukomaa kwa mwanamke na kufikisha umri wake unategemea kabisa utaratibu wa aina hii katika jamii.

Pia ni lazima kukumbuka kwamba wanawake wanaotahiri kikazi – mara nyingi ni wakunga wa kijijini – hivyo hawataki kupoteza mapato yao. Kwa sababu hii wanapinga kwa kila namna juhudi za kupinga tohara kwa wanawake.

## 4. Hali halisi

Baada ya zaidi ya karne moja ya vita dhidi ya ukeketaji, hebu tutafakari hali ilivyo sasa: hapakuwa na mafanikio makubwa. Hata mijini wasichana bado wanatahiriwa. Wasichana na kina mama wanajikuta katika hali ngumu za ki fikira, washindwe wawache utamadumi au wakubali kutahiriwa.

Kwa hiyo kuna mambo mawili muhimu:

(a) lazima kuwekwe utaratibu za kitamaduni wa jamii;

(b) lazima tohara ikatazwe / ipigwe marufuku.

## 4.1 Kutafuta suluhisho

Hali hii inayoonekana kujipinga, itawezaje kutatuliwa? - Kwa kawaida mila za asili katika jamii yoyote, zinatofautiana kwa namna tu. Kwa hiyo kwanza ni lazima tukubali kwamba utaratibu wa mila za asili upo. Kama tujuavyo, hilo ni jambo gumu kubadilishwa. Linalobaki ni kubadili muundo wake. Inavyoonekana ni hila hiyo tu yenye kutumainiwa. Lakini hatuna budi kuwa waangalifu tusibadili utaratibu kupita kiasi. Kwa mfano tukishauri kwamba mila za jamii zibadilishwe kuwa sherehe tu bila ukeketaji wa aina yeyote, tutazamie upinzani. Swala kama hili ni kusahau maana ya mfumo wa mila za asili. Tukiangalia jambo hili kinaganaga, tutagundua kwamba:

- Ni lazima zoezi hili lihusu kinembe,
- lazima kuwepo kukatwa,
- lazima damu itoke.

Sambamba na hoja hiyo,tusipokubali masharti hayo ya kiutamaduni, hatutafanikiwa – kama vile tumeona mpaka sasa. Tukilinganisha na jambo hili kwa wanaumme, swala la kuwepo sherehe bila zoezi au jaribio lenyewe haliwezi kukubalika.

Kuna uchaguzi gani katika uwanja wa masharti ya kiutamaduni? – Ili kujibu swali hili ni muhimu kuangalia aina tofauti za ”tohara kwa wanawake”. Mila zinaweza kuwa tofauti sana kutegemea mahali au nchi. Inavyoonekana utaratibu haukuwa mwingi sana katika muundo wa zamani wa Kiislamu. Siku hizi zoezi linafanyika ifuatavyo:

- kukatwa kwa ngovi cha kinembe tu,
- kukatwa kinembe kizima (clitoridectomy),
- kukeketwa au kukatwa kinembe na midomo midogo ya uke (*labiae minorae*),
- kukatwa na kushonwa kwa kinembe na midomo.

Tohara ya kukata ngozi ya kinembe ambayo hufanyika kwa nadra tu, haiathiri, na inafananishwa kama tohara ya mwanamume.[1] Lakini njia hiyo sio ya kawaida, na kwa upande mwingine ni tofauti ambapo uke mzima unaondolewa kikatili. Katika tamaduni nyingine za kiafrika majeraha yanashonwa au kushikizwa kwa miiba kwa njia isiyo safi. Wenye kutahariwa kwa njia hii wanateseka maisha yao yote na wanaweza kuambukizwa maradhi vibaya sana na hata kupoteza maisha.

Asilimia 2.5 tu za tohara ya uke zinazofanyika ni za aina isiyo na hatari. Sana zinafanyiwa ngozi ya uke au sehemu ndogo za kinembe. Tukiangalia zile nyingine asilimia 97.5 inamaanisha kuwa mamilioni ya wanawake ambao wanatahiriwa kwa njia kali wanaathiriwa kimwili na kiroho – ikiwa watapona baada ya. Balaa hili linahitaji kuingiliwa kati haraka.


## 5. Mbinu mpya

Ili kutimiza masharti ya kitamaduni na hata hivyo kutotahiri sehemu zenye maana sana, ustadi ufuatao unaweza kuwa ufumbuzi wa tatizo hili.


Juu ya kinembe hupatikana kigovi (*praeputium clitoridis*), na kutoka kigovi hiki hutoka kinyama (*glans clitoridis*) mara kwa mara. Hivyo huweza kufananishwa kigoni hiki na kile cha kiumme cha mboro (picha ya 1).

Ustadi huu mpya hujihusisha tu na kingozi cha kinembe, hakuna kitu kitaondolewa na zile sehemu zingine za uke haziwezi kudhuriwa kwa vyo vyo te.

[1] Kuhusu tohara ya uume ni lazima kukumbuka kwamba mume akitahiriwa hupunguza hatari ya mke kupata *cervical cancer*.



*Picha ya. 1: Picha inaonyesha uke uzima na ngovi (praeputium clitoridis), kinembe (glans clitoridis), midomo midogo (labiae minorae) na midomo mikubwa (labiae maiorae).*




*Picha ya 1 a: Kinembe na ngovi yake*




*Picha ya 1 b: Mkato wa kukingama wa kinembe na ngovi (sagittal plane)*

Kato lifanyike toka juu kwenda chini kwa kufungua kingozi tu na kutoa nje kinundu cha kinembe. (picha ya 2). Matokeo yake ni kuwa hii si tohara ya kawaida, ni kato la kingozi (*incisio praeputii*) tu. Hata hivyo inatimiza misingi ya matakwa ya mila za kiutamaduni: kuna kukatwa sehemu cha kigovu na kuna damu. Kuna utaratibu wa aina hii ambao hutumika katika bara la Asia kaskazini magharibi ambapo sehemu ya juu ya govi la uume hufunguliwa kwa kukatwa.[2]

[2] Utamaduni wa Mangyans kwenye kisiwa cha Mindoro (nchini Philippines)



*<u>Picha ya 2</u>: Mpango wa mstari wa kukata (mstari wa nukta)*



*<u>Picha ya 2 a</u>: Picha hiyo lakini kwa ukubwa na mpango wa mstari wa kukatwa (mstari wa nukta)*

Endapo utamaduni unalazimisha kukatwa kitu chochote, basi kigovu kidogo tu juu ya kinembe kiondolewe na

<u>ihakikishwe kwamba kinembe kisidhuriwe!</u>

Lakini kuna jambo jingine: Kwa wanawake wengi, kigovu cha kinembe ni kubwa kidogo, hadi kinembe hakiwezi kuonekana: Wakati wa nyege, kinembe hufura na kusimama kama mboro. Lakini kigovu kikiwa kubwa, kinembe yaweza kufunikwa. Kama kimefunikwa, kinembe hakiwezi kupata ule utamu wa kimapenzi.

Kwa wale wanawake wengi wanaosumbuliwa na aina hicho cha kigovu, njia mpya na IP (*incisio praeputii*) chaweza kuonwa kama faida. Si hivyo, hawawezi kupata uzuri wa kuguzwa kwa kinembe wakati wa kufanya mapenzi kutokana na kuzuiliwa na kigozi kikubwa. Hivyo,

<u>njia hii mpya inatatua shida ndogo badala ya kusababisha nyingine kubwa</u>.

## 5.1 Tahadhari

Ni busara kutumia dawa ya kuzuia maumivu (*xylocaine*). Hata hivyo IP inaweza kulinganishwa na jeraha dogo tu la ngozi. Lakini mambo kadhaa ni muhimu sana:

- Kukatwa kufanyike kwa chombo safi kabisa kinachofaa (bora kwa kisu cha kazi ya udaktari).
- Uangalifu wa hali ya juu uwepo ili kinembe kisidhurike, kwa sababu kiko hapo chini yake!
- Mara tu baada ya kukata jeraha lisafishwe kidawa. Kama dawa ya kusafisha haipo kinywaji chenye kileo (*alcohol*) kinaweza kutumika.
- Kupona kunaweza kutazamiwa baada ya siku chache (kama vile jeraha lolote jingine), hewa safi ni muhimu kwa jeraha kupona.[3]

Tuna sababu ya kutumaini kwamba IP itachukua nafasi ya kukeketa wanawake. Hivyo hatuwezi kuvumilia hatari ya kuambukizwa maradhi wakati wa kutekeleza jambo hili. Wale walio na mashaka kuhusu IP watapendelea kuendelea na tohara ya uke na watatafuta sababu za kila namna kupinga mkakati huu mpya.

---

[3] Kufungwa pamoja kwa miguu, kama ni kawaida katika sehemu fulani, lazima iepukwe na badala yake hewa safi lazima ifike kinonda. Hata waliotahiriwa wanaumme wana hatari ya hali ya juu; ambako siku hizi vyumba, ambapo lazima wabaki siku chache, hufuniwa na plastik badala ya matawi.

## 6. Mawaidha bora

Kama tulivyojifunza kupiga tu marufuku tohara ya wanawake hakutafanikiwa. Kwa hiyo ni lazima utumizi mpya wa IP utumie mbinu nyingine:

- Badala ya kukataza utaratibu wa mila, wale ngariba (kawaida ni wanawake wazee na mara nyingine ni wazalishaji) wanaopata riziki yao kwa njia hii, wapate lisensi rasmi kwa sheria – lakini inawapasa kutekeleza utaratibu kwa njia hii MPYA.
- Badala ya kuwatenga katika kuunda mbinu huu upya wakubaliwe na kushirikishwa.

Tumejifunza pia kuwa iwapo tutajaribu kufanya mabadiliko bila kujali miundo ya utamaduni, kuna hatari tohara kufanyika kisiri ”chinichini” katika sehemu zisizotambulika rasmi.

Hivyo kuifanya rasmi inamaanisha kuendelea kuwa na utawala.

Ubalozi kamili ni juu ya shirika za vijiji (local NGOs) na wanaojitolea. Wao wana ujuzi wa habari zote na wa hali halisi ya kitamaduni katika sehemu zile waliko. Yaweza kuwa bora ikiwa wanaotahiri watatangaza adharani kujitolea kwao ili wawajibike kufanya hivyo. Kuenezwa kwa mageuzo (mapinduzi) haya bora ni lazima kuambatane na kushirikishwa bora. Kwa sababu hii ingesaidia kuonyesha ustadi mpya vijijini na miundo ya uke ama na picha zenye kueleza wazi ni nini kinakusudiwa ili kuepuka kutoeleweka. Bila shaka kwa kutafsiri neno kwa vitendo, kunatakiwa usimamizi (mwongozo). Ikiwezekana, ingefaa kuhudhuria utaratibu huu mpya wa mila wenyewe.

Katika mijadala na wanawake wanaoshikilia utamaduni wao, imeonekana inafaa kuwaambia, ”Mungu amemuumba mwanamke hivyo, kwa kuwa ndivyo alivyotaka awe. Na sasa unaharibu kile alichoumba Mungu kwa mapenzi yake!” Hoja hii inaweza kusaidia kuwashauri watu hawa angalau wasiharibu vinembe vya binti zao (au hata vyao vyenyewe).

Hata hivyo kuna umuhimu wa mbinu za usimamizi:

⇒ Ni lazima kuhakikisha IP ifanyike ipasavyo na bila kudhuru kinembe chenyewe.

⇒ Wasichana wakaguliwe zaidi ya mara moja baada ya IP ili izuiliwe kukeketwa na wengine baadaye

Kama mapinduzi/mageuzo ya mila/desturi yatafanikiwa, lazima yakubaliwe kuwa jambo la kufaa na sawa kwa thamani kuchukua nafasi ya yale yaliokuwa yanatendwa mpaka sasa. Yaani: watu wanaohusika wasitafakari kwamba mabadiliko haya ni kupotea kwa utamaduni. Lazima ielezwe wazi – hasa kwa wasichana, lakini pia kwa watu wengine wanaohusika – kwamba njia hii mpya ya kuhusisha kukatwa kidogo tu inafaa kabisa kupitisha usichana kuwa uke na kwamba inatekeleza kabisa jando iliyokusudiwa.

## 7. Matazamio

Kwa kutekelezwa kisheria shughuli ya mapinduzi/mageuzo, angalau mijini, ingehamishwa kuwa chini ya sehemu ya utibabu. Hata hivyo iwe wazi kabisa kwamba kile kinachofanyika Misri (angalia hapa juu) hakipatani na elimu ya maadili ya tibabu. Badala ya kuwatahiri wasichana kwa ukatili hospitalini, madaktari wenyewe wawajibike na kutumia nafasi hii kwa kukomesha tohara ya uke. Ikiwa idara za serikali zitakataa kuhusika kabisa, tohara ya uke itaendelea katika sehemu zisizotambulika rasmi, kama tulivyoona. Lakini umuhimu wa mila ikitambuliwa, mapinduzi/mageuzo yatamaanisha kwamba badala ya kupiga marufuku kungekuweko uwezekano rasmi wa kutekeleza hatua mpya hospitalini (ambayo pia ingekuwa mfano wa kuigwa sehemu za vijijini). Matokeo yangekuwa mwisho wa wanawake kuteswa kutokana na tohara ya kikatili. Badala yake kungekuwa na vitu vyema -

- dawa ya kufanya mtu asione maumivu (anaesthesia) ,
- kupunguka sana kwa maambukizo,
- hapatakuwa na madhara ila hali itakuwa bora katika hali ya kujamiana,
- na hata hivyo, utamaduni rasmi.

Kwa siku za usoni yangekuwa ni mabadiliko katika desturi hii.

## 8. Majibu

Kwa kuihimiza bora njia hii mpya katika vita dhidi ya tohara ya uke, inabidi ienezwe, watu waelimike kutokana na mazoea na ifanywe bora zaidi kinagaubaga. Kwa hiyo unakaribishwa siyo tu kukopi na kusambaza makala hii, bali pia kuitafsiri katika lugha nyingine kufuatana na mahitaji, kama muandiko na pia kaseti. Lakini hasa kukusanya habari:

– kukubaliwa kwa jambo ili;
– njia bora ya kuwahelimisha watu kuihusu;
– upatanishi;
– uangalifu wa upasuaji (kwa kukata kingovu);
– masharti ya kuponyesha;
– n.k.

Ukitaka kuiunga mkono shughuli hii ya mapinduzi/mageuzo, tafadhali tuma habari zote (tafsiri, data, picha n.k.) kwa:

Dr. Arnold Groh
Laubenheimer Str. 36
D-14197 Berlin
simu/fax: +49+30-8227854
e-mail: a.groh@berlin.de

Hivyo mchango wako unaweza kusaidia kufadhilisha toleo lijalo la maelezo haya na kuafiki hila hii vizuri iwezekanavyo. Kwa ujumla, lengo ni kuzuia ukatili usiendelee.

Tukifikiria wasichana wote wanaotahiriwa kila siku hakuna wakati wa kupoteza –

tenda kazi sasa!

© A. Groh, 1999-2002
Makala haya yanaruhusiwa kuchapishwa, kutafsiriwa na kusambazwa, lakini tu yakiwa yote kwa jumla. Tafadhali nakala ya kila tafsiri itumwe kwa anwani ya mwandishi hapa juu.

Utafsiri na Eva Guddat, Varel/Germany na Lawrence Mutwol (kutoka Marakwet, Kenya), Freie Universität Berlin

Translation by Eva Guddat, Varel/Germany and Lawrence Mutwol (from Marakwet, Kenya), Free University of Berlin